**Raslimali za Lugha ya Kiswahili**

Karibu kwenye Maktaba! Springfield-Greene County Library District imefunguliwa kwa watu wote katika jamii yetu. Mwongozo huu ni utangulizi wa rasilimali za maktaba zinazopatikana kwa wateja wanaozungumza Kiswahili, ikiwa ni pamoja na huduma za tafsiri, jinsi ya kupata na kufikia nyenzo na utafiti wa lugha ya Kiswahili na rasilimali za jamii.

Tazama Video ya Kukaribisha ya Maktaba na utambulishwe kwa Maktaba na huduma zote inazotoa.

- **Kuhusu Maktaba** (pdf)

Je, unahitaji kadi ya maktaba? Kuja na fomu iliyojazwa, kitambulisho cha picha, na ithibati ya anwani kwenye tawi lolote la maktaba au Maktaba Itembeayo.

- **Fomu ya Kujiandikisha kupata Kadi ya Maktaba (pdf)**

**Huduma za Utafsiri**
Maktaba inatoa huduma za utafsiri ili kusaidia katika kuwasiliana na wateja. Tafadhali mjulishe mhudumu ikiwa unahitaji mtafsiri.

**Jifunze Kiingereza**
Mango Languages ni programu ya kufurahisha na rahisi ya kujisomea mtandaoni ili ujifunze Kiingereza. Unaweza kuitumia bila malipo ukitumia kadi yako ya maktaba. Unaweza kuanza kujifunza sasa hivi kwa kuchagua 'Guest Access' (Ufikiaji wa Mgeni) au unaweza kuunda nenosiri ili kila unaporudi kwenye ukurasa, unaweza kuendelea pale ulipoachia.

**Nyenzo kwa Lugha ya Kiswahili**
Maktaba hutoa nyenzo katika lugha kadhaa. Tafadhali zungumza na mhudumu kwa taarifa zaidi.

**Raslimali za Jamii**

**City of Springfield: Tume ya Meya ya Haki za Binadamu na Mahusiano ya Jamii**
Inashirikiana na jamii ili kukuza maelewano na heshima kati ya makundi yote ya rangi, dini na makabila na kuzuia ubaguzi dhidi ya makundi hayo yanayolindwa na Sheria ya Jiji; inachunguza madai ya matukio ya ubaguzi na inajaribu kupatanisha wahusika ili kupata suhulu; inawezesha ubadilishanaji wa maelezo kuhusu haki za binadamu, na inatoa huduma zake kusaidia kuelimisha raia na vikundi vya kijamii.

Busch Municipal Building
840 Boonville Ave.
Springfield, MO 65802
417-864-1038

**International Institute -Tawi la Southwest Missouri**
Inawasaidia wakimbizi na wanaotafuta kimbilio.

1114 E Commercial St, Springfield, MO 65803
417-720-1552

## Raslimali za Biashara

**Maktaba ya Springfield-Greene County**
Maktaba ya Springfield-Greene County inatoa huduma kwa biashara yako ndogo au kubwa kupitia raslimali za mtandaoni, mipango ya wataalamu wa biashara na usaidizi wa moja kwa moja. Wafanyakazi waliobobea watakusaidia kupata maktaba na rasilimali bora zaidi za jamii ili uanzishe na ukuze biashara yako. Huduma za Maktaba kwa Mahitaji ya Biashara Yako [pdf]

Maeneo mbalimbali katika Kaunti yote ya Greene
417-882-0714
Muulize Mkutubi

**Multicultural Business Association** *(hapa awali ilijulikana kama Minorities in Business)*
Inasaidia kuanzisha na kukuza biashara zinazomilikiwa na wachache na kutoa mwongozo kwa rasilimali za eneo, jimbo na serikali ya shirikisho.

405 N. Jefferson Ave
(Inapatikana katika eFactory)
Springfield, MO 65806
417-837-2631
sgfmib@gmail.com

**International Institute of Southwest Missouri**
Hutoa huduma za biashara na ukuzaji wa mali ikiwa ni pamoja na mikopo midogo, mikopo inayosaidia kuimarisha uwezo wa mtumiaji wa kupata mikopo mikubwa, na kuwasaidia wajasiriamali wanawake.

1114 E Commercial St, Springfield, MO 65803
417-720-1552
info@iistl.org

**eFactory**
Inasaidia biashara zinazoanzishwa ili kukua, ni kituo cha rasilimali, na mtandao wa usaidizi katika Southwest Missouri Lengo lao ni kutumika kama kituo kimoja cha raslimali zote kwa wamiliki wote wa biashara ndogo wa kusini magharibi mwa Missouri. Wanawasaidia wajasiriamali kutafuta usaidizi wa mija kwa moja au waajiri wakubwa kushughulikia changamoto za wafanyakazi.

Inapatikana katika Robert W. Plaster Free Enterprise Center
405 N Jefferson Ave, Springfield, MO 65806
417-837-2600

**MOSourceLink**
Wanajulikana kama mfumo wa ikolojia wa ujasiriamali katika Missouri. Lengo lao ni kurahisisha ujasiriamali na kuifanya Missouri kuwa jimbo la uvumbuzi katikati mwa nchi. MOsourceLink iliundwa kama mtandao wa mapendekezo wa jimbo zima unaounganisha wamiliki wa biashara wa Missouri na rasilimali za eneo, kanda, vyuo vikuu na jimbo. Wapigie simu Wasaidizi wao wa Mitandao ili wakuunganishe na rasilimali na kukuza biashara yako.

4747 Troost Ave.
Kansas City, MO 64110
866-870-6500
Watumie barua pepe moja kwa moja

## Raslimali za Uraia

**Sherehe za Uandikishaji wa Uraia, Wilaya ya Magharibi**
Mahakama ya Wilaya ya Marekani ya Wilaya ya Magharibi ya Missouri imebaki na mamlaka ya pekee ya kuendesha sherehe za uandikishaji wa uraia kwa waombaji wanaotaka uraia. Sherehe hizi husimamiwa na Jaji wa Wilaya ya Marekani, Hakimu wa Masuala ya Usimamizi, au Jaji wa Ufilisikaji na kimsingi hufanyika katika mahakama ya Jiji la Kansas.

Charles Evans Whittaker U.S. Courthouse
400 E. 9th Street
Kansas City, MO 64106
816-512-5000

**Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani**
USCIS ni shirika la serikali linalosimamia uhamiaji halali nchini Marekani.

**Somea Mtihani (toleo la mwaka wa 2008)**
Maelezo ya Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani ili kusaidia kusoma kwa ajili ya mtihani.

## Raslimali za Lugha ya Kiingereza

**Mango Languages** kutoka kwa Maktaba
Mango Languages ni huduma ya kujifunza lugha inayotolewa na Maktaba bila malipo kwa watu wanaomiliki kadi za maktaba. Moja ya kozi zinazotolewa kwa Kiingereza ni kwa wazungumzaji wa Kihispania wa Amerika ya Kusini.

Maeneo mbalimbali katika Kaunti yote ya Greene
417-883-5341
Muulize Mkutubi

**Mpango wa English Connections - Taasisi ya Lugha ya Kiingereza - Chuo Kikuu cha Missouri**
Jifunze Kiingereza nyumbani na uungane na watu kutoka kote ulimwenguni. Mpango wa English Connections hukusaidia kuimarisha ujuzi wote nne wa Kiingereza: Kuandika, Kusoma, Kusikiliza na Kuzungumza katika darasa la mtandaoni la kufurahisha na jumuishi. Hulipishwi kuhuduhuria.

901 S. National Ave
Springfield, MO 65897
417-836-5000
info@missouristate.edu

**Mipango ya Mtandaoni ya ELI - Taasisi ya Lugha ya kiingereza - Chuo Kikuu cha Jimbo la Missouri**
Taasisi ya Lugha ya Kiingereza katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Missouri inatoa mipango ya mtandaoni ya kujifunza lugha ya Kiingereza. Hulipishwi kuhuduhuria.

901 S. National Ave
Springfield, MO 65897
info@missouristate.edu

**Baraza la Ozarks Literacy**
Linawasaidia wanafunzi wa umri wowote na mafunzo ya mtu binafsi ya kusoma bila malipo.

Midtown Carnegie Branch Library (Lower Level)
397 E. Central St.
Springfield, MO 65802
417-616-0505
info@ozarksliteracy.org

**Chuo cha Ozarks Technical Community: Elimu na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika kwa Watu Wazima**
Kinatoa madarasa na mafunzo ya bila malipo katika elimu ya msingi na ujuzi wa kusoma na kuandika kwa watu wazima, maandalizi ya mtihani wa HSE, na masomo ya Kiingereza kama Lugha ya Pili.

221 Graff Hall
725 E. Bob Barker Blvd.
Springfield, MO 65802
417-447-8860
ael@otc.edu

**Mkusanyiko wa Raslimali za Ujuzi wa Kusoma na Kuandika kwa Watu Wazima wa Maktaba ya Springfield-Greene County**

Kwenye Maktaba, aina mbalimbali za mada za dhahania na halisi kwa wanafunzi watu wazima huitwa Mkusanyiko wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika kwa Watu Wazima (Adult Literacy Collection). Vitabu hivi huangazia stadi za maisha, upishi, wasifu wa historia za watu binafsi, namna ya kujisaidia, kupanga bajeti, hadithi za kudhahania za watu wazima, na majina ya watoto kwa mtu mzima anayejifunza. Tafuta orodha kwa "literacy collection."

Maeneo mbalimbali katika Kaunti yote ya Greene
417-883-5341
Muulize Mkutubi

## Raslimali za Dini

**Redeemed Christian Church of God (Covenant House)**
Lina maono ya kufikia na kuhudumia jamii yenye tamaduni nyingi inayokua haraka katika Springfield, MO.

1349 W Meadowmere St. Springfield, MO 65804
417-719-8802
rccgspringfieldmo@gmail.com

**Kanisa la Life360 Intercultural Church**
Kanisha mshirika wa Assemblies of God Church lenye kituo chake cha uongozi katika Springfield, Missouri. Kanisa huandaa hafla ambapo washirika huleta chakula cha jioni vya asili mbalimbali za kimataifa kila Jumamosi ya nne ya kila mwezi.

2220 W Chesterfield St, Springfield, MO 65807
417-447-9000
info@life360.org

## Raslimali za Usaidizi wa Kisheria

**Kituo cha Hand in Hand Multicultural Center**
Usaidizi wa kisheria wa uhamiaji uliothibitishwa na kuidhinishwa na Ofisi ya Haki, kutoa hati, tafsiri, ushauri wa kitaalamu, ushauri wa ndoa na familia. Unapata huduma za ukalimani ukiweka miadi. Mipango na maonyesho ya kitaalamu ya jamii kwa afya ya akili, uhamiaji, afya ya familia, na mipango inayozingatia watu wanaozunguma lugha mbili, makabila madogo na watu wasiojiweza. Huduma zinapatikana katika lugha nyingi tofauti yaani Kihispania, Kiromania, Kichina, Kimandarini, Kikantonisi, Kihmong, Kikorea, Kivietinamu, Kiburma na nyinginezo.

Je, una tatizo? Pigia simu Hand in Hand kwa ushauri wa dakika 15 ili kujadili tatizo na watajaribu kukupa mwongozo.

P.O. Box 1577
Springfield, MO 65801
417-865-4673

jhumphrey@hihmc.org

**Huduma za Kisheria katika Southern Missouri**

Hutoa uwakilishi wa bila malipo wa kisheria kwa wateja wa kipato cha chini katika baadhi ya matatizo ya kisheria ya kiraia; haitoi uwakilishi wa utetezi wa jinai; inashughulikia kesi zinazohusu misaada ya umma, makazi, malipo ya ukosefu wa ajira, familia, elimu ya watumiaji, ajira, afya na masuala mengine.

809 N. Campbell Ave.
Springfield, MO 65802
1-800-444-4863 (bila malipo)
417-881-2159

**Pata Ofisi ya USCIS**

Hutoa usaidizi wa kuunganishwa na rasilimali zinazotolewa na Serikali ya Shirikisho. Viungo vilivyo hapo chini vinaonyesha jinsi ya kupata ofisi za eneo kwa ajili ya mahojiano ya maombi kwa wahamiaji na wanaotafuta kimbilio.

## Raslimali za Shule za Umma

**Uandikishaji katika Shule za Umma za Springfield**

Hutoa hatua za jinsi ya kuandikisha wanafunzi kwenye Wilaya ya Shule za Umma ya Springfield. Ombi la Mtandaoni la Kujiandikisha.

Kraft Administrative Center
1359 E. St. Louis St. Springfield, MO 65802
417-523-0000

**Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELL) / Ukuzaji wa Lugha ya Kiingereza**

Mafundisho ya ELD yameundwa ili kuwasaidia wanafunzi kutoka tamaduni na lugha tofauti kujifunza na kujua Kiingereza hadi kiwango cha ufasaha ambacho huongeza uwezo wao wa kushiriki kwa mafanikio katika masomo ya kitaaluma yanayofundishwa kwa Kiingereza.

Roseann Bentley Administrative Center
1610 E. Sunshine Springfield, MO 65804
417-523-1136